Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

# Nje Bulletin

Toleo Na: 01 | Aprili 2021



Tanzania, Afrika Kusini zaahidi kuendeleza ushirikiano



## Tanzania, kufanya mageuzi ya Kidiplomasia

# Tahariri


Timu ya Uhariri

Mhariri Mkuu
Emmanuel Buhohela

Mhariri Msaidizi
Sheiba Bulu

Wachangiaji
Rosemary Malale
Ally Kondo
Rose Mbilinyi
Teodos Komba
Nelson Kessy

Usanifu
KItengo cha Mawasiliano



Mawasiliano:
Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Afrika Mashariki
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba
40466 , Dodoma, Tanzania.
S.L.P. 2933, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255-26- 2323201-7
Baruapepe: nje@nje.go.tz
dodoma@nje.go.tz


## Tuongeze juhudi kukukuza Diplomasia ya Uchumi

Diplomasia ya Uchumi imekuwa ni uelekeo mpya wa kisera hususani Sera ya Mambo ya Nje kwa mataifa mengi duniani katika kuendeleza ushirikiano wake na mataifa mengine. Hii ni kufuatia kumalizika kwa harakati za kukomboa mataifa kutoka katika ukoloni pamoja na kupungua kwa kiasi kikubwa kwa mitazamo ya migogoro ya kivita miongoni mwa mataifa.

Hali hiyo imeyafanya mataifa kutafakari namna bora ya kusimamia maslahi ya wananchi na kuwa na uhusiano wenye tija na mataifa mengine kwa kuangalia faida za kiuchumi zinazopatikana na kuziwezesha pande zote zinazohusika katika uhusiano huo wa kidiplomasia zinanufaika.

Kwa kutambua hilo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nayo iliandaa na kutumia Sera ya Mambo ya Nje inayozingatia Diplomasia ya Uchumi ili kupata maslahi ya msingi ya taifa na kuwawezesha wananchi wake kupiga hatua za kimaendeleo.

Sera ya Mambo ya Nje imezingatia kupanga, kukuza na kulinda maslahi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa uendelevu wa diplomasia ya uchumi na kuhakikisha kuwa mahusiano mazuri ya Tanzania na Mataifa mengine na taasisi za kimataifa yanazingatia maslahi ya kiuchumi pamoja na kudumisha amani na usalama.

Katika kuzingatia hilo, Serikali ya Awamu ya Sita ikiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imeona ni vyema suala la diplomasia ya uchumi kuwekwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 - 2025 ambapo pamoja mambo mengine, CCM itaihimiza Serikali kuendelea kushiriki kwenye utengamano wa kikanda na kuendeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuzingatia maslahi muhimu ya nchi yetu ili kunufaisha Watanzania wote.

Diplomasia ya uchumi inachangia katika kuharakisha utangamano wa kisiasa na kiuchumi na kijamii kwa kuweka mazingira muhimu yatakayoiwezesha Tanzania kushiriki kwa ukamilifu katika majadiliano ya kikanda na kimataifa.

Mataifa mengi duniani kwa kutambua suala hilo, yamebadilisha uelekeo wa kutoka katika diplomasia ya zamani iliyokuwa inalenga zaidi kutekeleza masuala ya kisiasa na kuelekea kwenye utekelezaji wa diplomasia ya uchumi inayosisitiza kuboresha na kuendeleza maslahi mapana ya kiuchumi.

Kwa kuzingatia maslahi ya wananchi, Serikali ya Awamu ya Sita, imeendelea kujikita zaida kwenye diplomasia ya uchumi ikiwa ni mkakati mojawapo wa Nchi kushirikisha mataifa ya kigeni kujinufaisha kiuchumi katika sekta za biashara na uwekezaji, kilimo, utalii, elimu, afya, mikopo ya riba nafuu na kupata teknolojia ya kisasa.

Aidha, Tanzania imeweza kusonga mbele katika kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kukuza biashara ya uwekezaji kwa kiasi kikubwa kwa mfano; biashara kati ya Tanzania na Saudi Arabia imekuwa ikiimarika kukuwa ambapo mpaka sasa miradi 14 ya uwekezaji kutoka nchini humo imesajiliwa katika kituo cha taifa cha uwekezaji (TIC) huku kampuni nane za Kitanzania zikipata kibali cha kuuza minofu ya samaki nchini humo.

Kadhalika, Tanzania na China zimekuwa zikishirikiana katika mkakati wa kukuza mauzo ya bidhaa za Afrika nchini China ikilenga kuleta faida za kiuchumi kwa pande zote mbili ambazo zinasaidia kuinua uchumi na biashara katika sekta za biashara, uwekezaji, fedha, kilimo, nishati, viwanda, utalii, madini na miundombinu ambazo zimekidhi viwango na ubora unaokubalika katika soko la kimataifa.

Pamoja na mambo mengine, ni vyema Tanzania kuendelea kujikita katika kuhamasisha diplomasia ya uchumi ili kuwezesha uchumi wake kuimarika na kusonga mbele.

Julai Mosi 2020, Benki ya Dunia iliitangaza rasmi Tanzania kuingia katika uchumi wa kipato cha kati ikiwa ni miaka mitano kabla ya muda uliokuwa unatarajiwa kwa Serikali kuingia katika uchumi wa kati, ikiwa ni pamoja na jitihada za utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyobuni ajira kwa watanzania wengi jambo ambalo lililoipelekea Benki ya Dunia kuitangaza Tanzania kama taifa lenye kipato cha kati.





*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge kutoa mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita Aprili 22, 2021 Jijini Dodoma*

# Tanzania Yapania Mageuzi Makubwa Mahusiano ya Kimataifa

**Serikali** ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imepania kufanya mageuzi katika mahusiano na ushirikiano wa kimataifa kwa kutekeleza shughuli za kidiplomasia kwa ufanisi zaidi ili kuendana na utekelezaji wa sera ya Diplomasia ya Uchumi

Akihutubia Bunge la 12 Jijini Dodoma Jana Rais Samia aliuelezea umma wa Watanzania kuwa Serikali yake imejipanga kuendeleza mahusiano na Ushirikiano na Mataifa mengine na Taasisi za Kidunia, Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga kutekeleza shughuli za Kidiplomasia kuendana na Sera ya Diplomasia ya Uchumi.

"Tumekusudia kuimarisha na kukuza Uhusiano na Mataifa mengine pamoja na jumuiya za kikanda na Taasisi za Kimataifa," Amesema Mhe. Rais Samia

Mhe. Rais ameongeza kuwa ili kutimiza azma hiyo, Serikali inakusudia kuimarisha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Balozi zetu zilizoko nchi mbali mbali duniani, kwa kuajiri watumishi wenye sifa na weledi wa kazi na kusambaza vitendea kazi, pamoja na kutumia kiuchumi.....

..............**Inaendea Uk 6**



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan*

# Tanzania, Afrika Kusini zaahidi kuendeleza uhusiano



*Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Liberata Mulamula (Mb) akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Jamhuri ya Afrika Kusini, Mhe. Grace Naledi Pandor*

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Liberata Mulamula amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Jamhuri ya Afrika Kusini, Mhe. Grace Naledi Pandor kujadili mambo ya kuendeleza mashirikiano baina ya Jamhuri ya Afrika Kusini na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Balozi Mulamula amefanya mazungumzo hayo Pretoria nchini Afrika Kusini ambapo pamoja na mambo mengine, Balozi Mulamula alieleza kuwa mahusiano kati ya Afrika Kusini na Tanzania ni ya kihistoria na yameendelea kuimarika tangu enzi a kupigania uhuru kwa nchi za kusini mwa Afrika.

Kwa upande wake Waziri Pandor ameishukuru kwa ujio wa Balozi Mulamula na kwa kufika nchini Afrika Kusini na pia alieleza kuwa Jamhuri ya Afrika Kusini inathamini mashirikiano ya kihistoria kati ya nchi zetu mbili na hivyo kinachohitajika ni kuendeleza na kuimarisha mashirikiano ya kiuchumi na kisiasa tuliyonayo sasa hivi. Jamhuri ya Afrika Kusini inayo azma ya kushiriki kikamilifu kujenga makumbusho ya urithi (heritage museum) ya harakati za kupigania uhuru kusini mwa Afrika zenye chimbuko lake nchini Tanzania na vilevile kuonyesha juhudi za Tanzania katika harakati za kupigania uhuru na kwa nchi za kusini mwa Afrika.

Mawaziri hao wamejadili pia mchakato wa tathimini ya utekelezaji wa Bi-National Commission (BNC) ambapo kwa mwaka huu Afrika Kusini ndiyo itakuwa mwenyeji wa tathimini hiyo ambayo hujumuisha ngazi ya watedaji wakuu wa sekta mbalimbali wan chi hizi mbili, Mawaziri na huitimishwa na Waheshimiwa Marais wa nchi zote mbili.

Aidha, Balozi Mulamula kabla ya kukutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini, alikutana na watumishi wa ubalozi wa Tanzania Pretoria katika mkutano ulifanyika Ubalozini, Mhe. Waziri alipokea taarifa ya eneo la uwakilishi la Ubalozi ambalo linajumuisha Afrika Kusini, Botswana, Falme ya Lesotho na SADC. Taarifa hiyo ilieleza juhudi za Ubalozi katika kukuza mahusiano na nchi za eneo la uwakilishi, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, diplomasia ya siasa, wanadiaspora wa eneo la uwakilishi.

Balozi Mulamula ameutaka Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini kuendela kufanya kazi kwa malengo, watumishi kujiwekea malengo ili kufanikisha malengo ya Ubalozi na hatimaye Ubalozi kuchangia malengo ya Wizara kwa ujumla.

"Nawasihi kuendeleza mahusiano na nchi za uwakilishi na Balozi nyingine zilizopo katika nchi za uwakilishi na suala hili la kujenga mahusiano na watumishi wote na siyo Balozi pekee yake," amesema Balozi Mulamula.



*Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Liberata Mulamula (Mb) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini Mhe. Meja Jenerali (Mst) Gaudence Milanzi pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Ubalozi wa Tanzania nchini humo*

# Balozi Ibuge aridhishwa na uendeshwaji wa Miradi ya Maji Mwanza



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge (kulia) akimsikiliza Mtendaji wa Sekretarieti ya Bonde la Ziwa Victoria Dkt. Ally Said Matano (kushoto) wakati akiwasilisha mpango mkakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Bonde hilo*



*Sehemu ya Wadau kutoka sekta mbalimbali wakifuatilia uwasilishwaji wa mpango mkakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Bonde la Ziwa Victoria uliokuwa ukifanywa na Mtendaji wa Sekretarieti ya Bonde hilo Dkt. Ally Said Matano*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge akisisitiza jambo kwa wafanyakazi wa Bonde la Ziwa Victoria (Hawapo Pichani) baada ya uwasilishwaji wa mkakati wa utekelezaji wa mpango miradi katika Bonde la Ziwa Victoria*

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge ameeleza kuridhishwa kwake na ubunifu na uendeshwaji wa miradi mbalimbali ya maji na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabia Nchi katika Bonde la Ziwa Victoria. Miradi hiyo inatekelezwa chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC).

Balozi Ibuge kwenye ziara hiyo akiwa ameambatana na wataalamu kutoka Sekta ya Maji, Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Wataalumu kutoka LVBC, amebainisha kuwa lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kutambua maendeleo ya Miradi inayotekelezwa katika ukanda wa Ziwa Victoria ambayo inawagusa wananchi zaidi ya milioni 40 kutoka Nchi Tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kubaini changamoto zilizopo ili kutoa suluhisho linalofaa.

Akizungumza wakati akihitimisha ziara hiyo Katibu Mkuu Balozi Brigedia Jenerali Ibuge ameongeza kueleza kuwa asilimia kubwa ya Ziwa Victoria ipo Tanzania (kwa 51%) hivyo, Serikali ya Jumhuri ya Muungano wa Tanzania inayapa kipaumbele kinachostahili masuala yote ya maendeleo yanayoendelea katika Ziwa hilo sambamba na masuala ya kiusalama. "Serikali inafanya kazi kubwa sana ya kutengeneza meli kubwa za usafirishaji na uvuvi ili kuwezesha maendeleo ya wananchi na kuhakisha usalama wao wakati wote wakiwa wanatekeleza majuku yao" amasema Balozi Ibuge.

Wakati huohuo Balozi Brigedia Jenerali Ibuge amepokea taarifa ya mpango mkakati wa utelezaji wa miradi mbalimbali katika Bonde la Ziwa Victoria, iliyowasilishwa na Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Bonde hilo Dkt. Ally Said Matano. Sambamba na uwasilishaji wa taarifa hiyo Dkt. Matano ametoa rai kwa Serikali ya Tanzania kuendelea kutoa ushirikiano kwa LVBC katika kutekeleza majukumu yake ambayo yanalenga kuboresha maisha ya wana Afrika Mashariki.

LVBC ni Taasisi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye Makao Makuu yake Kisumu, Kenya. Taasisi hii ilianzishwa ili kuratibu maendeleo endelevu na usimamizi wa Bonde la Ziwa Victoria katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambapo nchi hizo zililitaja Bonde hilo kuwa eneo la "maslahi makubwa ya kiuchumi na eneo la ukuaji wa uchumi wa Kikanda litakaloendelezwa kwa pamoja na Nchi wanachama wa Jumuiya.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge kutoa mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita Aprili 22, 2021 Jijini Dodoma*

# ....Mageuzi Makubwa Mahusiano ya Kimataifa

*Inatoka Uk ......3*

Kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji mzuri wa Diplomasia ya Uchumi, Serikali pia imekusudia kuboresha na kusimamia majengo na viwanja ambavyo ni mali ya Tanzania vilivyoko nje ya nchi.

Hayo yalibainishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati alipokuwa akihutubia Bunge la 12 Jijini Dodoma Jana ambapo pamoja na mambo mengine aliweza kutoa mwelekeo wa Serikali yake.

"Naomba kuwahahikishia kuwa tutafungua na kuanzisha pia Balozi mpya, Konseli pamoja na Vituo vya Biashara kwenye nchi na miji ya kimkakati ili kutangaza vivutio vyetu vya utalii, kuvutia uwekezaji na kutafuta masoko ya bidhaa zetu," Amesema Rais Samia.

Rais Samia ameongeza kuwa Serikali anayoiongoza imekusudia kufanya uchambuzi wa kitaalamu utakaobaini nafasi ya kila ofisi ya ubalozi katika kukuza biashara, uwekezaji na utalii. Uchambuzi huo ndio utatumika kupanga maafisa kulingana na uwezo wa kila Ubalozi.

"Tutaendelea kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kimataifa, ikiwemo ushiriki wetu kwenye kulinda amani duniani. Tunakusudia pia kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2000 ili iendane na mahitaji ya sasa ya dunia," ameongeza Rais Samia.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (Kulia) mara baada ya kulihutubia Bunge Aprili 22, 2021 Jijini Dodoma*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi mara baada ya kulihutubia Bunge Aprili 22, 2021 Jijini Dodoma*

# Anglogold Ashanti, Tanzania zakubaliana kuendeleza ushirikiano



*Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Liberata Mulamula (Mb) akizungumza na Afisa Mtendaji Mkuu wa Anglogold Ashanti – Afrika, Bw. Sicelo Ntuli wakati walipokutana kwa mazungumzo leo jijini Dar es Salaam*

Kampuni ya Madini ya Anglogold Ashanti ya Afrika Kusini imeahidi kuendeleza ushirikiano na Serikali ya Tanzania katika sekta ya madini na kuhakikisha kuwa sekta hiyo inakuwa mstari wa mbele kuchangia uchumi.

Ahadi hiyo imetolewa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Anglogold Ashanti - Afrika, Bw. Sicelo Ntuli wakati alipokutana kwa mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Liberata Mulamula (Mb) leo Jijini Dar es Salaam.

Akiongea mara baada ya mazungumzo hayo Balozi Mulamula amesema kuwa, Anglogold Ashanti ni wadau wakubwa katika sekta ya madini na wameonesha utayari wao wa kushirikiana kwa karibu na Serikali katika kukuza na kuendeleza sekta ya madini.

"Leo hii nimekutana na uongozi wa Kampuni ya Madini ya Angogold Ashanti na tumejadili pamoja na mambo mengine, utayari wa Kampuni hiyo kushirikiana na Serikali katika kukuza sekta ya madini hapa nchini," Amesema Balozi Mulamula

Balozi Mulamula ameongeza kuwa kitendo cha kukutana na wadau wa madini kama Anglogold Ashanti na kujadiliana nao masuala mbalimbali ya ushirikiano wa kukuza sekta ya madini ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya Diplomasia ya Uchumi.

Kwa Upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu



wa Anglogold Ashanti Bw. Ntuli amesema kuwa uongozi wa Anglogold umefarijika kukutana na Mhe. Waziri wa Mambo ya Nje na kuweza kujadiliana nae mambo mbalimbali ikiwemo suala la kukuza ushirikiano baina ya Kampuni hiyo na Serikali ya Tanzania.

"Sisi kama Anglogold tumefarijika kuona Serikali ya Tanzania ipo tayari kuendeleza ushirikiano na Sisi.......tunaahidi kuendeleza ushirikiano huu kwa maslahi mapana ya pande zote mbili," Amesema Bw. Ntuli

Aprili 16, 2021 Kampuni ya Anglogold Ashanti iliingia ubia na Kampuni ya BG Umoja ya nchini Tanzania kwa ajili ya kuchimba madini katika miradi ya Nyankanga na Geita Hill. Anglogold ni Kampuni mama ya Geita Gold Mine (GGML) imeipatia BG Umoja mkataba wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 186 kwa miaka miwili.

**"Leo hii nimekutana na uongozi wa Kampuni ya Madini ya Angogold Ashanti na tumejadili pamoja na mambo mengine, utayari wa Kampuni hiyo kushirikiana na Serikali katika kukuza sekta ya madini hapa nchini,"**



*Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Liberata Mulamula (Mb) akiongoza kikao chake na Kampuni ya Madini ya Anglogold Ashanti ya Afrika Kusini kilichofanyika leo jijini Dar es Salaam*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mkuu wa Itifaki (Chief of Protocol) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Yusuph Tindi Mndolwa kuwa Balozi katika hafla fupi iliyofanyika katika Ikulu ya Chamwino, Dodoma*

# Rais Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mkuu wa Itifaki

